JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# MWONGOZO WA TAIFA WA UENDESHAJI, USIMAMIZI NA URATIBU WA MABARAZA YA USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDOA

**MEI, 2023**



# MWONGOZO WA TAIFA WA UENDESHAJI, USIMAMIZI NA URATIBU WA MABARAZA YA USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDOA

MEI, 2023

# YALIYOMO


DIBAJI ....................................................................................................iv

SHUKRANI ....................................................................................................v

VIFUPISHO VYA MANENO ....................................................................................vi

TAFSIRI YA MANENO ....................................................................................vii

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI .................................................................................... 1

1.0. Maelezo.................................................................................... 1
1.1. Usuli.................................................................................... 1
1.2. Chimbuko la Mwongozo .................................................................................... 2
1.3. Umuhimu wa Mwongozo .................................................................................... 2
1.4. Malengo ya Mwongozo .................................................................................... 2
1.5. Mfumo wa Sheria wa Usimamizi wa Ndoa .................................................................................... 3
1.6. Maudhui ya Sheria ya Ndoa .................................................................................... 3
1.7. Walengwa na Watumiaji wa Mwongozo.................................................................................... 6
1.8. Mchakato wa kuandaa Mwongozo .................................................................................... 6
1.9. Mpangilio wa Mwongozo.................................................................................... 6

SEHEMU YA PILI
MUUNDO, WAJUMBE NA MAJUKUMU YA MABARAZA YA USULUHISHI WA NDOA .................................................................................... 7

2.1. Maelezo.................................................................................... 7
2.2. Muundo wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa .................................................................................... 7

SEHEMU YA TATU
UTARATIBU WA USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDOA .................. 12

3.1. Maelezo.................................................................................... 12
3.2. Maadili na Kanuni za Kuzingatiwa na Mabaraza .................................................................................... 12
3.3. Taratibu za Uendeshaji wa Usuluhishi wa Ndoa .................................................................................... 12
3.4. Hatua za Uendeshaji na Usuluhishi wa Ndoa .................................................................................... 13
3.5. Ratiba ya Vikao vya Usuluhishi.................................................................................... 13
3.6. MAOMBI YA TALAKA MAHAKAMANI.................................................................................... 13

## SEHEMU YA NNE
## MAJUKUMU YA WADAU ........................................................................ 14

4.1. Maelezo........................................................................................................................14
4.2. Majukumu....................................................................................................................14
4.3. Wasaidizi wa Kisheria/Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii.......................................................19
4.4. Msajili wa Vizazi na Vifo (RITA)...................................................................................19

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI SHIRIKISHI, UFUATILIAJI NA TATHMINI................................ 20

5.1. Maelezo........................................................................................................................20
5.2. Usimamizi Shirikishi .......................................................................................................20
5.3. Ufuatiliaji ......................................................................................................................20
5.4. Utoaji wa Taarifa ...........................................................................................................20
5.5. Tathmini........................................................................................................................20

## VIAMBATISHO.......................................................................................... 21

6.1. Fomu Na.1. Fomu ya Wito ............................................................................................21
6.2. Fomu Na.2: Pingamizi la Ndoa.........................................................................................22
6.3. Fomu Namba 3: Rufaa Mahakamani.................................................................................23

## MSIMBO/KIELELEZO.................................................................................. 25

# DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua na kuthamini mchango wa Taasisi ya ndoa katika kudumisha amani, upendo na utulivu kwenye familia na jamii ili kuchangia maendeleo ya Taifa. Pamoja na mchango mkubwa wa Taasisi hii, katika siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la migogoro ya ndoa na familia inayosababisha madhara kwa wanandoa, watoto, jamii na Taifa kwa ujumla. Miongoni mwa madhara hayo ni pamoja na kuvunjika kwa ndoa, watoto kukosa malezi bora, kuongezeka kwa vitendo vya unyanyasaji, ukatili wa kijinsia, na ukatili dhidi ya watoto. Hali hii imesababisha kurudisha nyuma juhudi za familia, jamii na Taifa katika kujiletea maendeleo.

Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali katika kukabiliana na kutafuta suluhu ya migogoro ya ndoa nchini kupitia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mipango ya kisekta. Baadhi ya juhudi hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008),Sheria ya Mtoto(2009) Sheria ya Ndoa Sura ya 29 na Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura ya 206. Aidha, Sheria ya Ndoa inatambua Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Mabaraza ya Usuluhishi ya Jumuiya. Mabaraza hayo yamepewa mamlaka ya kusikiliza na kusuluhisha migogoro ya ndoa kwa lengo la kuboresha na kuimarisha mahusiano katika ndoa na familia.

Serikali imeandaa Mwongozo huu kwa lengo la kuimarisha uendeshaji, usimamizi na uratibu wa utoaji wa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Mwongozo huu unaainisha Muundo, Majukumu ya Mabaraza, Mfumo wa Uendeshaji, Majukumu ya Wadau katika ngazi mbalimbali na kufanya usimamizi shirikishi, ufuatiliaji na tathmini.

Tunatoa rai kwa mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa  na wadau wote wanaohusika na utekelezaji wa Mwongozo huu kuusoma kwa makini, kuuelewa na kuutumia ipasavyo ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya kuboresha na kuimarisha mahusiano katika ndoa, familia, jamii na Taifa kwa ujumla.



Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)
**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**



Anjellah J. Kairuki (Mb)
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI**



Dkt. Damas Ndumbaro(Mb)
**Waziri wa Katiba na Sheria**

## SHUKRANI

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ushirikiano wa wadau mbalimbali. Hivyo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWM) inapenda kutoa shukrani kwa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Wizara ya Afya (WA), Wizara ya Katiba na Sheria (WKS), Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi – Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto na Mahakama ya Tanzania. Vilevile, Wizara inatoa shukrani kwa Wadau wa Maendeleo, Taasisi za Elimu ya Juu, Taasisi za Dini, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, wajumbe wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa ikiwemo Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya kutoka Mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam. Aidha, tunatoa shukrani kwa wawakilishi wa Mabaraza ya Jumuiya kutoka Kanisa Katoliki (RC), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri - Tanzania (KKKT), Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa Anglikana Tanzania (ACT) na Viongozi wa Mila, kwa mchango mkubwa walioutoa katika kukamilisha Mwongozo huu.

Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa msaada wa kitaalaam na kifedha katika kuandaa na kukamilisha Mwongozo huu. Kipekee, Wizara inatoa shukrani kwa Bi. Anna Henga - Mkurugenzi Mtendaji, Bw. Fulgence Massawe - Mkurugenzi wa Utetezi na Maboresho na maafisa wengine wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wakiwemo Bi. Getrude Dyabene, Bi. Rose Nyatega, pamoja na Bw. Raymond Kanegene kwa kushiriki kikamilifu katika kuandaa Mwongozo huu.

Wizara inathamini na kutambua mchango wa Dkt. Zainabu A.S. Chaula aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kusimamia mchakato wa uandaaji wa Mwongozo huu. Aidha, Wizara inatambua mchango wa kikosi kazi cha wataalam kilichoshiriki kuandaa Mwongozo huu wakiongozwa na Dkt. Nandera E. Mhando, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Bw. Baraka P. Makona na Bw. Tullo S. Masanja – Makamishna Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii, Bw. Shilungu E. Ndaki – aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali watu - Bi. Visensia Kagombora, Mkurugenzi wa Sera na Mipango - Bw. Sayi Magessa, Mratibu wa Mwongozo - Bi. Asia P. Jingu na maafisa wengine wa Wizara. Vilevile, tunathamini mchango wa Dkt. Joyce Nyoni - Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW), Dkt. Abu Mvungi - Mhadhiri Mwandamizi - Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW), Dkt. Thomas Ndaluka – Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Mhe. Mwajuma Lukindo – Hakimu Mkazi Mfawidhi Mahakama ya Wilaya Kondoa, Bi. Lilian E. Kilembe kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Insp. Mwanaidi Lwena kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani - Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto na Bi. Neema Kweka kutoka OR– TAMISEMI.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinatambua mchango wa wadau wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha mchakato mzima wa kuandaa na kukamilisha Mwongozo huu.



Dkt. John A.K. Jingu
**Katibu Mkuu - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| ACT | Anglican Church of Tanzania (Kanisa Anglikana Tanzania) |
| BAKWATA | Baraza Kuu la Waislam Tanzania |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es salaam |
| ISW | Institute of Social Work (Taasisi ya Ustawi wa Jamii) |
| KKKT | Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania |
| KUJ | Kamishna wa Ustawi wa Jamii |
| LHRC | Legal and Human Right Centre (Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu) |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MTUNF | Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa na Familia |
| MSM | Mamlaka ya Serikali za Mitaa |
| Na. | Namba |
| OR - TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OUT | Open University of Tanzania (Chuo kikuu Huria cha Tanzania) |
| RC | Roman Catholic (Kanisa Katoliki) |
| RITA | Registration Insolvency and Trusteeship Agency (Msajiliwa Vizazi na Vifo) |
| WA | Wizara ya Afya |
| WKS | Wizara ya Katiba na Sheria |
| WMJJWM | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |
| WMN | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi |
| WMTH | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari |

# TAFSIRI YA MANENO

***Baraza la Kamishna***
Ni baraza linaloundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kifungu cha 102 kwa ajili ya usuluhuishi wa migogoro ya ndoa.

***Familia***
Ni kikundi cha watu wenye ujamaa na wanaoishi pamoja ambao ni baba, mama, watoto na ndugu wengine. Kikundi hicho mara nyingi ni sehemu ya kundi kubwa zaidi la ukoo linalounganisha watu wenye asili moja katika uzazi wa pamoja.

***Fomu Na. 1***
Ni fomu ya wito wa wanandoa kufika kwenye Baraza la Usuluhishi wa Ndoa .

***Fomu Na. 2***
Ni fomu ya pingamizi la Ndoa inayokusudiwa kufungwa.

***Fomu Na. 3***
Ni fomu maalum inayotumika kuwasilisha shauri Mahakamani baada ya kushindikana kwa usuluhishi katika ngazi ya Mabaraza.

***Kamishna***
Kwa mujibu wa Mwongozo huu, ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

***Kutengana***
Ni hali ya wanandoa kuishi mbalimbali kufuatia kukosekana kwa maelewano baina yao kwa kukubaliana au kwa amri ya mahakama.

***Mabaraza ya Kata***
Ni mabaraza yaliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3. Cha Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura 206.,

***Mabaraza ya Jumuiya***
Ni mabaraza yenye mamlaka juu ya jumuiya mbalimbali zikiwemo taasisi za dini na za kimila zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria kufanya kazi ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa.

***Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa***
Ni mabaraza ambayo yamewekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 Kifungu cha 102 kwa ajili ya kusuluhisha wanandoa walio katika mgogoro.

***Mgogoro wa Ndoa***
Ni pale panapotokea kutokuelewana kati ya wanandoa kunakosababisha kukosekana kwa maelewano na amani katika ndoa.

***Ndoa***

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa Sura ya 29 Ndoa ni muunganiko wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa maisha yao yote.

***Ndoa inayobatilika***

Hii ni ndoa ambayo ni halali lakini ina matatizo yanayoweza kusababisha mwanandoa mmojawapo kuomba ndoa ivunjwe.

***Rejista***

Kwa mujibu wa Mwongozo huu, ni rejista ya usuluhishi wa Mashauri ya Ndoa

***Talaka***

Talaka ni hati inayotolewa na mahakama baada ya kuthibitisha kuvunjika kwa ndoa

***Usuluhishi wa migogoro ya Ndoa***

Ni jitihada zinazofanyika katika kuwawezesha wanandoa kutatua tofauti zao ili waweze kudumisha ndoa yao katika hali ya amani.

# SEHEMU YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.0. Maelezo

Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa vipengele kumi (10) muhimu vya Mwongozo. Vipengele hivyo vinajumuisha: usuli; mfumo wa Sheria na Usimamizi wa ndoa na familia; maudhui ya Sheria ya Ndoa; chimbuko; umuhimu; malengo; walengwa; watumiaji; na mpangilio wa Mwongozo huu.

## 1.1. Usuli

Ustawi wa taasisi ya Ndoa ni muhimu katika kuimarisha huduma za familia, watoto, maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Serikali kwa kutambua umuhimu wa taasisi hii, ilitunga Sheria ya Ndoa Sura ya 29 ya Mwaka 1971 iliyofanyiwa marejeo Mwaka 2019 na kanuni zake ili kuweza kusimamia masuala ya ndoa na ustawi wa familia. Katika kutekeleza jukumu hilo Sheria ya Ndoa kifungu cha 102, inampa mamlaka Waziri wa Katiba na Sheria kuunda Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa. Hivyo, mabaraza yanayoundwa kwa mujibu wa sheria hii ni pamoja na Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya jumuiya yanayojumuisha mabaraza ya kimila na ya kidini na Mabaraza ya Kata. Lengo la Mabaraza haya ni kuhakikisha ustawi wa ndoa na familia kwa kutoa huduma za usuluhishi na upatanishi kwa wanandoa pale panapojitokeza migogoro inayohatarisha ustawi wa taasisi ya ndoa.

Mwaka 1971 Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria alitangaza Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa. Miongoni mwa Mabaraza hayo ni Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Jumuiya na Mabaraza ya Kata ambayo pamoja na majukumu mengine yamekasimiwa kusuluhisha migogoro ya ndoa kwa mujibu wa sheria. Huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii hupokea mashauri ya ndoa kutoka katika makundi yote ya jamii. Mabaraza ya Jumuiya hupokea mashauri kutoka kwa wanajumuiya wa jamii husika kwa kuzingatia imani za dini na mila za jamii hiyo. Aidha, Mabaraza ya jumuiya hutoa huduma ya usuluhishi katika ngazi mbalimbali kulingana na muundo wa kitaasisi uliowekwa kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya ndoa. Kwa mfano, katika dini ya Kiislam, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa yapo kuanzia ngazi ya Kata, Wilaya, Mkoa na Makao Makuu ya jumuiya ya Kiislam. Vilevile, kwa upande wa madhehebu ya kikristo, mabaraza yanaundwa kwa ngazi kwa kuzingatia utaratibu wa dhehebu husika. Mabaraza ya Kata yapo kila kata nchi nzima na hupokea mashauri ya wanandoa katika kata husika.

Ili Baraza la Usuluhishi wa Ndoa liwe na uhalali linapaswa kutambuliwa na kuidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya sheria ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali kama ilivyotamkwa na Sheria ya Ndoa sura ya 29 Kifungu cha 102.
Aidha, tangu kutungwa kwa Sheria ya Ndoa, Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa yameendelea kusuluhisha migogoro ya ndoa pasipo kuwa na Mwongozo mahsusi wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Vilevile, zipo changamoto za ukiukwaji wa taratibu za kisheria katika usuluhishi wa migogoro ikiwemo mabaraza kutokufahamu mipaka ya kazi zake, kutumia wajumbe wasio na sifa katika mabaraza, kutoa hukumu badala ya kusuluhisha, ndoa kusuluhishwa bila kuwa na mabaraza halali na uelewa mdogo wa taratibu za uendeshaji wa migogoro ya ndoa na taratibu za kutoa rufaa.

Hivyo, kutokana na mapungufu hayo, Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kuweza kujibu changamoto za usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika Mabaraza yanayotambuliwa na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kama ilivyofanyiwa marejeo Mwaka 2019. Mwongozo huu utawezesha kuwa na uelewa wa pamoja wa taratibu na kanuni za kushughulikia migogoro ya ndoa ili kuimarisha mahusiano kwa wanandoa, familia na watoto, pamoja na kuzuia vitendo vya ukatili na unyanyasaji katika ndoa, familia na jamii kwa ujumla.

## 1.2. Chimbuko la Mwongozo

Ndoa hufungwa kwa lengo la wanandoa kuishi pamoja na kujenga familia yenye furaha, amani, upendo na maendeleo. Hata hivyo, ndoa nyingi hukumbwa na migogoro ambayo isiposuluhishwa mapema husababisha wanandoa kutengana na kuvunjika kwa ndoa. Vilevile, migogoro ya ndoa isiposuluhishwa mapema husababisha uwepo wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto. Hali hii husababisha watoto kukosa matunzo na malezi stahiki katika familia. Aidha, usuluhishi wa ndoa na familia unafanywa na serikali katika ngazi mbalimbali na katika mabaraza ya ndoa lakini tumebaini kuwa kukosekana kwa Mwongozo wa Taifa unaoweka utaratibu wa kufuatwa katika mchakato wa usuluhishi unasababisha kutokuwepo kwa mfanano wa utoaji wa huduma katika mabaraza hayo na ukiukwaji wa sheria na kanuni zinazosimamia usuluhishi wa Ndoa.

Ustawi wa ndoa ni muhimu katika kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii. Kwa kuzingatia hili, Wizara kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii inalo jukumu la kusimamia na kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa, familia na mahusiano kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM). Hivyo, Mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020 Kifungu cha 93 (L) katika kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030, Afrika Tuitakayo 2063, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Miaka Mitano wa Maendeleo (2020 - 2025) ambao ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) ambao pamoja na mambo mengine mipango hiyo ina lengo la kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii kwa kutoa kipaumbele katika kuimarisha uchumi wa kaya, kuimarisha mahusiano na ustawi wa jamii, familia na watoto.

## 1.3. Umuhimu wa Mwongozo

Huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa zimekuwa zikitolewa bila mwongozo wa utoaji wa huduma hii; hivyo kusababisha utoaji wa huduma kufanywa bila kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni mbalimbali. Kwa kuliona hili, Serikali imeandaa Mwongozo utakaotumika katika kutoa huduma zote za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na kuongeza uelewa wa mabaraza ili kuwezesha huduma za usuluhishi kutolewa kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizokubalika kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa na kanuni zake.

## 1.4. Malengo ya Mwongozo

### 1.4.1. Lengo Kuu

Kuimarisha uendeshaji, usimamizi na uratibu wa utoaji wa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa.

### 1.4.2. Malengo Mahsusi

i. Kuweka mfumo utakaotumiwa na wataalam, wajumbe wa mabaraza na wadau wa masuala ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa, familia na mahusiano ili watoe huduma kwa kuzingatia taratibu na sheria;
ii. Kuhakikisha kuwa mabaraza yote yanaendeshwa kwa kufuata muundo wa mabaraza ya usuluhishi na kanuni za usuluhishi;
iii. Kuimarisha utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
iv. Kuwajengea uwezo wataalam na wajumbe wa mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa, familia na mahusiano ya ndoa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kwa utaalam; na
v. Kutoa elimu ya mahusiano kwa familia na jamii ili kupunguza vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa wanandoa na watoto.

## 1.5. Mfumo wa Sheria wa Usimamizi wa Ndoa

Nchini Tanzania masuala ya ndoa yanaendeshwa na kusimamiwa kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Sheria na Kanuni zinazosimamia huduma hizi ni pamoja na Sheria ya Ndoa, Sura ya 29; ambapo Kifungu cha 102 kimetoa Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa, na Kifungu cha 103(1) kinaelekeza muundo wa mabaraza hayo. Sheria zingine zinazosimamia haki na ustawi wa ndoa na familia ni pamoja na Sheria ya Mtoto, sura ya 13 na kanuni zake ambazo zinatoa mwongozo wa matunzo ya watoto kupitia huduma ya usuluhishi wa wazazi na wanandoa ili kutoa matunzo stahiki kwa watoto. Vilevile, Sheria ya Mabaraza ya Kata, sura 206, imekasimu Mabaraza ya kata kusuluhisha migogoro ya ndoa. Pia Sheria ya Vinasaba vya Binadamu Na. 8 ya Mwaka 2009 inasaidia wanandoa/wazazi kufikia makubaliano kuhusu uhalali wa mzazi wa mtoto, na Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya Mwaka 2017 ambayo imetambua wasaidizi wa Msaada wa Kisheria kutoa msaada wa kisheria kwenye masuala ya ndoa.

## 1.6. Maudhui ya Sheria ya Ndoa

Sehemu hii inatoa tafsiri na kuainisha taratibu mbalimbali zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ikiwemo maana ya ndoa; aina za ndoa, taratibu za kufungisha ndoa, wajibu wa wanandoa, sifa za wanandoa, ndoa inayobatilika, maana ya familia, talaka na sababu zinazosababisha ndoa kuvunjwa na Mahakama.

### 1.6.1. Maana ya Ndoa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Ndoa Sura 29, Ndoa ni muunganiko wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke uliokusudiwa kudumu kwa maisha yao yote.

### 1.6.2. 1.6.2 Aina za Ndoa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(2) na (3) cha Sheria ya Ndoa kuna aina mbili tu za ndoa zinazotambulika ambazo ni:-

i. Ndoa ya mke mmoja; na
ii. Ndoa ya wake wengi.

### 1.6.3. Taratibu za Kufungisha Ndoa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1), cha sheria ya Ndoa Sura ya 29 kuna aina tatu za ufungishaji ndoa ambazo ni kidini, Kiserikali na kimila:-

i. **Kidini:** Hii ni ndoa inayofungwa kwa taratibu za dini mbalimbali kama vile Kikristo, Kiislam au dini nyingine kwa kufuata taratibu za madhehebu husika.
ii. **Kimila:** Hufungwa kwa kufuata mila na taratibu za jamii husika; na
iii. **Kiserikali:** Ndoa hii hufungwa mbele ya Afisa wa Serikali mwenye mamlaka ya kufungisha ndoa.

### 1.6.4. Sifa za Ndoa

i. **Hiari:** Lazima kila mmoja wa wanandoa awe ameridhia kwa hiari yake kamili bila hila kutumika, kulaghaiwa au kulazimishwa na mtu yoyote;
ii. **Jinsi:** Lazima wawe watu wawili wa jinsi tofauti, mmoja wa kiume na mwingine wa kike;
iii. **Wasiwe maharimu**, yaani wasiwe na undugu wa damu;
iv. **Wanaotazamiwa** kufunga ndoa wasiwe wamewekewa pingamizi; na
v. **Umri:** Kwa kuzingatia Sheria zilizopo na maslahi ya mtoto.

### 1.6.5. Haki na Wajibu wa Wanandoa

i. Kushiriki tendo la ndoa;
ii. Mke kupata matunzo kutoka kwa mume na isipokuwa pale ambapo mume hana uwezo kwa sababu ya ugonjwa au ulemavu;
iii. Mume kutunzwa na mke pale ambako mume hana uwezo huo kutokana na ugonjwa, ugonjwa wa afya ya akili na ulemavu;
iv. Kumiliki mali (ya ndoa au binafsi);
v. Kutunza siri za unyumba, isipokuwa vitendo vya ukatili; na
vi. Haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa.

### 1.6.6. Ndoa inayobatilika

Hii ni ndoa ambayo ni halali lakini ina matatizo yanayoweza kusababisha Mwanandoa mmojawapo kuomba ndoa ivunjwe. Zifuatazo ni miongoni mwa sababu zinazoweza kusababisha ndoa kuwa batilifu: -

i. Endapo mwanandoa mmoja hawezi tendo la ndoa;
ii. Endapo mmojawapo ana ugonjwa wa afya ya akili;
iii. Endapo mwanandoa amepata mimba kutoka kwa mtu mwingine mbali ya mwanaume aliyemuoa; na
iv. Endapo tendo la ndoa halifanyiki kwa kuwa mwanandoa amekataa kufanya hivyo kwa makusudi.

### 1.6.7. Kutengana na Talaka

Kutengana na talaka ni haki alizonazo kila mwanandoa endapo ndoa yao itakuwa na matatizo kiasi kwamba itaonekana wazi kuwa wawili hawa hawawezi kuendelea kuishi pamoja.

#### 1.6.7.1. Kutengana

Kutengana ni ile hali ya wanandoa kuacha kuishi pamoja, yaani kuacha kuishi chini ya dari moja.

#### 1.6.7.2. Aina za Kutengana

Kutengana kupo kwa aina mbili:-

i. Kutengana kwa hiari; na
ii. Kutengana kwa amri ya Mahakama.

### 1.6.8. Talaka

Mahakama ndio chombo pekee chenye uwezo wa kuvunja ndoa. Ni lazima talaka itolewe na Mahakama ili haki ya kila mwanandoa itamkwe bayana.

Kwa mujibu wa kifungu cha 100 cha Sheria ya Ndoa, Mahakama haiwezi kusikiliza shauri la talaka kama ndoa haijadumu kwa miaka miwili. Ili shauri la talaka lipokelewe kabla ya miaka miwili ya ndoa kupita ni lazima Mahakama itoe idhini. Idhini hiyo hutolewa pale tu ambapo mwanandoa mmoja anapata mateso yasiyo ya kawaida.

### 1.6.9. Sababu za Talaka

Vifungu vya 99 na 107(2(a-g)) vya Sheria ya Ndoa vinatamka kwamba sababu inayoweza kufanya Mahakama kutoa talaka ni pale tu inapojiridhisha kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika. Zifuatazo ni sababu zinazofanya ndoa ionekane kuwa haiwezi kurekebishika tena: -

i. Ugoni;
ii. Mlalamikiwa kuacha kufanya tendo la ndoa
iii. Ukatili;
iv. Kutotimiza wajibu kwa makusudi;
v. Kutelekeza ndoa kwa makusudi;
vi. Kifungo cha maisha au kisichopungua miaka mitano;
vii. Kutengana kwa hiari au kwa amri ya Mahakama kwa muda usiopungua miaka mitatu;
viii. Kubadili dini; na
ix. Magonjwa ya afya ya akili yasiyopona ambayo madaktari bingwa wasiopungua wawili wamethibitisha kwamba hakuna uwezekano wa huyo mtu kupona.

### 1.6.10. Uwasilishwaji wa Shauri la Talaka Mahakamani

Kwa mujibu wa Kifungu cha 101 cha Sheria ya Ndoa mwombaji anatakiwa kabla ya kwenda kufungua shauri lake Mahakamani, ni lazima kwanza apeleke shauri lake katika Baraza la Usuluhishi, kwani kwa kushindwa kufanya hivyo kutafanya mahakama kushindwa kusikiliza shauri lake. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa imetoa mazingira ambayo hayamlazimishi mlalamikaji au mwombaji kupita katika baraza kutokana na sababu zifuatazo:

i. Kutelekezwa na mwenza na asijue mahali alipo;
ii. Pale mwenza anapoishi nje ya nchi na hakuna uwezekano wa kurejea ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kufungua shauri la talaka;
iii. Pale ambapo mlalamikiwa ameshindwa kufika katika Baraza la Usuluhishi kwa makusudi;
iv. Kifungo cha maisha au kifungo cha zaidi ya miaka mitano;
v. Pale itakapothibitika ana ugonjwa wa afya ya akili usiotibika; na
vi. Pale ambapo Mahakama itakapothibitisha kuwa kuna mazingira yasiyo ya kawaida na yanazuia kufika kwenye Baraza.

## 1.7. Walengwa na Watumiaji wa Mwongozo.

Mwongozo huu utatumika na Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa ikiwemo Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya; pamoja na Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma ikiwemo ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mahakimu, Kamati za Maendeleo ya Kata, watunga sera, watafiti, wadau wa maendeleo, wakuza mitaala na watoa huduma nyingine za kijamii.

## 1.8. Mchakato wa kuandaa Mwongozo

Maandalizi ya Mwongozo huu yamepitia hatua mbalimbali ambazo ni:-

i. Kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia masuala ya ndoa, familia na watoto;
ii. Kuunda kikosi kazi cha Wizara kilichohusika katika kuandaa mkutano wa kujadili na kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali;
iii. Kufanya kikao na wadau mbalimbali wa masuala ya Ndoa, Familia na watoto kwa ajili ya kujadili na kupokea maoni.
iv. Katika hatua ya nne, rasimu ya Mwongozo huu ilifanyiwa majaribio ili kujiridhisha na ukamilifu na ufanisi wake;
v. Hatua ya tano ilikuwa ni uwasilishaji wa Mwongozo katika ngazi ya Menejimenti ya Wizara ili kupokea maoni na umiliki; na
vi. Hatua ya mwisho ni kusainiwa kwa Mwongozo kwa ajili ya matumizi ya Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa na matumizi ya umma kwa ujumla.

## 1.9. Mpangilio wa Mwongozo

Mwongozo huu una sehemu kuu tano; ambapo sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili inaainisha muundo, wajumbe na majukumu ya Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa. Sehemu ya tatu inabainisha utaratibu wa usuluhishi wa Ndoa. Sehemu ya nne inaainisha mgawanyo wa majukumu na sehemu ya tano ni usimamizi shirikishi, ufuatiliaji na tathimini ya utendaji wa Mabaraza.

# SEHEMU YA PILI
# MUUNDO, WAJUMBE NA MAJUKUMU YA MABARAZA YA USULUHISHI WA NDOA

## 2.1. Maelezo

Sehemu hii inaainisha Muundo wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa katika ngazi tofauti kama ambavyo Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 na Matangazo ya Serikali Na. 196, Na. 211 na Na. 245 ya Mwaka 1971; ambayo yametamka uanzishwaji wa Mabaraza ya Ndoa katika ngazi tofauti ambazo ni Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Kata ya Usuluhishi wa Ndoa na Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa ya Jumuiya, kama inavyosimamiwa na miongozo ya masuala ya ndoa. Aidha, Mabaraza hayo yameainishwa Kisheria kama ifuatavyo:-

i. Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
ii. Mabaraza ya Kata ya Usuluhishi wa Ndoa; na
iii. Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa ya Kijumuiya.

## 2.2. Muundo wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, sura ya 29 Kifungu cha 103 (1) kila Baraza la Usuluhuishi la Ndoa lazima liwe na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua wawili (2) na wasiozidi watano (5). Hivyo, Muundo unaowasilishwa hapa umezingatia matakwa ya kisheria na unabainisha viongozi, wajumbe, sifa za wajumbe pamoja na majukumu ya wajumbe kulingana na aina ya Baraza kama ilivyofafanuliwa na sheria ya Ndoa sura ya 29 Kifungu cha 103(2)(a)(b).

### 2.2.1. Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii

a. Muundo wa Baraza

Baraza hili linaundwa na wajumbe wafuatao:-

i. Mwenyekiti;
ii. Makamu Mwenyekiti;
iii. Wajumbe wengine wanne watakaoteuliwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

b. Sifa za Wajumbe

i. Mwenyekiti wa Baraza atakuwa ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
ii. Makamu Mwenyekiti atakuwa ni Afisa Ustawi wa Jamii mwenye cheo cha uandamizi na kuendelea;

**Zingatio:** Sifa za wajumbe wengine zitategemea Matakwa ya Kamishna wa ustawi wa Jamii aliyepewa mamlaka ya uteuzi kama ilivyotangazwa katika tangazo la serikali namba 196(2)

c. Majukumu ya Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii

i. Kufanya unasihi kwa wanandoa walio kwenye migogoro na mafarakano ili kupata suluhu ya matatizo yanayowakabili na kuwawezesha kuishi kwa amani na upendo;
ii. Kufanya ufuatiliaji wa makubaliano yaliyofikiwa na wanandoa katika usuluhishi;
iii. Kutoa elimu kwa wanandoa/familia kwa lengo la kuwapa stadi za kuboresha mahusiano;

iv. Kuelekeza mashauri ya ndoa katika Mahakama pale inapobidi kwa kujaza Fomu Na. 3 kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Ndoa;
v. Kujaza kwenye Rejista taarifa zote muhimu na kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa za mashauri yote ya Baraza kwa Katibu Mkuu; na
vi. Kufanya kazi kama itakavyoelekezwa na sheria nyingine yoyote itakayotungwa na Bunge inayohusiana na masuala ya ndoa na familia.

**d. Majukumu ya Katibu**

i. Kupokea mashauri na kuyasajili kwenye Rejista ya Mabaraza ya Ndoa;
ii. Kuandaa taarifa;
iii. Kuandaa mhutasari wa kikao;
iv. Kutunza kumbukumbu za vikao kwa mujibu wa taratibu za utunzaji wa nyaraka za umma; na
v. Kujaza Fomu Na. 3 kadri itakavyoelekezwa na Baraza.

**e. Muda wa Wajumbe Kukaa Madarakani**

Wajumbe wa Baraza la Kamishna isipokuwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Mabaraza ya Jumuiya watatumikia nafasi hiyo kwa miaka mitatu; lakini wanaweza kuteuliwa tena kama mamlaka ya uteuzi itaona inafaa. Endapo mjumbe ataachishwa ujumbe kwa kukosa sifa kama zilivyoelezwa hapo juu, mjumbe mwingine atateuliwa kujaza nafasi hiyo na atatumikia kwa muda uliobaki. Hata hivyo, mjumbe huyu anaweza kuteuliwa kwa kipindi kingine.

**f. Uwajibikaji wa Baraza**

Katika kutekeleza majukumu yake, Baraza la Kamishna litawajibika kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na Ustawi wa Jamii. Hata hivyo nakala za taarifa za usuluhishi wa migogoro zitapelekwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria.

### 2.2.2. Mabaraza ya Kata ya Usuluhishi wa Ndoa

Baraza la Kata limeanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura 206. Wajumbe wa Baraza la Kata watapatikana kupitia Kamati ya Maendeleo ya Kata kutangaza nafasi hizo katika Vijiji/Mitaa kwa kushirikiana na wenyeviti wa Vijiji/Mitaa na watu wataomba nafasi hizo. Halmashauri ya Kijiji/Mtaa itachuja majina na kupata wawakilishi wawili kutoka kila Kijiji/Mtaa kwa kuzingatia jinsi na majina hayo yatawasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata ambako watachujwa na kupata wajumbe kulingana na Sheria ya Ndoa, sura ya 29 inavyoelekeza.

**a. Muundo**

i. Mwenyekiti;
ii. Makamu Mwenyekiti;
iii. Katibu atakuwa sehemu ya Baraza lakini haruhusiwi kutoa maoni;na
iv. Wajumbe watano ambao wawili lazima wawe wanawake.

**Kumbuka:** Akidi ya kikao cha usuluhishi ni wajumbe watatu kati yao angalau mwanamke awe mmoja.

**b. Sifa za Wajumbe wa Baraza la Kata**

i. Asiwe Mbunge;
ii. Asiwe mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata;

iii. Asiwe mjumbe wa Serikali ya Kijiji au Kamati ya maendeleo ya Kata Mtaa;
iv. Asiwe mwanasheria au mtumishi wa Mahakama;
v. Asiwe mtumishi wa Umma
vi. Asiwe na umri chini ya miaka 18;
vii. Asiwe na matatizo ya afya ya akili;
viii. Asiwe mtu ambaye amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai au kukiuka maadili; na
ix. Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**c. Sifa za Katibu**

i. Awe ameteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata;
ii. Awe amethibitishwa na Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji;

**Angalizo**- Asiwe mjumbe na haruhusiwi kutoa maoni

**d. Muda wa Wajumbe Kukaa Madarakani**

Wajumbe wa Baraza la Kata watadumu kwa muda wa miaka mitatu (3) lakini wanaweza kuchaguliwa tena. Endapo mjumbe ataachishwa ujumbe kwa kukosa sifa kama zilivyoelezwa hapo juu, mjumbe mwingine atateuliwa kujaza nafasi hiyo na atatumikia kwa kipindi kilichobaki na anaweza kuteuliwa tena. Katibu wa Baraza atakuwa ni Afisa wa Serikali aliyeteuliwa na mamlaka husika.

**e. Majukumu ya Baraza la Kata**

i. Kuimarisha amani na utengamano katika eneo lake la kazi kwa kuhakikisha migogoro inasuluhishwa kwa njia ya mazungumzo na kukubaliana;
ii. Kupokea na kusuluhisha mashauri ya migogoro ya ndoa;
iii. Kuandaa na kutoa barua ya wito;
iv. Kuendesha usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa;
v. Kutoa unasihi kwa wanandoa katika eneo husika;
vi. Kuelimisha wanandoa kuhusu malezi chanya ili kuimarisha makuzi na maendeleo ya mtoto katika familia;
vii. Kuwaeleza wanandoa haki na wajibu wao katika familia;
viii. Kusimamia makubaliano yaliyofikiwa na wana ndoa katika usuluhishi ili kuimarisha mahusiano baina yao, familia na watoto;
ix. Kuelekeza mashauri ya ndoa Mahakamani pale inapobidi kwa kujaza Fomu Na. 3 kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Ndoa;
x. Kujaza kwenye Rejista taarifa zote muhimu na kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa za mashauri yote ya Baraza kwa mamlaka husika; na
xi. Kufanya kazi kama ilivyoelekezwa na sheria nyingine zilizotungwa na Bunge, taratibu na mila za jamii husika.

**Kumbuka:** Katibu ndiye mwandishi wa vikao vya Baraza la Kata lakini hatakuwa sehemu ya maamuzi ya Baraza.

**f. Majukumu ya Katibu**

i. Kupokea mashauri na kuyasajili kwenye Rejista ya Mabaraza ya Ndoa;
ii. Kuandaa taarifa;

iii. Kuandaa muhtasari wa kikao;
iv. Kutunza kumbukumbu za vikao kwa mujibu wa taratibu za utunzaji wa Nyaraka za Umma; na
v. Kujaza Fomu Na. 3 na kuiwasilisha kwa Mwenyekiti kwa ajili ya kusainiwa.

**g. Uwajibikaji wa Baraza la Usuluhishi la Kata**

Katika kuhakikisha Baraza linafanya kazi yake kwa ufanisi litapaswa kuwajibika kwa Kamati ya Maendeleo ya Kata na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kila robo mwaka. Mkurugenzi wa Halmashauri/Jiji/Manispaa atawasilisha taarifa hiyo OR-TAMISEMI ambayo pia nakala yake itawasilishwa Wizara ya Katiba na Sheria (WKS).

**h. Uhifadhi wa Nyaraka**

Nyaraka zote na taarifa za usuluhishi zihifadhiwe katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata kwa utaratibu unaotumika kuhifadhi nyaraka za Serikali.

### 2.2.3. Mabaraza ya Jumuiya

Mabaraza ya Jumuiya ni Mabaraza yenye mamlaka juu ya Jumuiya mbalimbali zikiwemo taasisi za dini na kimila zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kufanya kazi ya Usuluhishi wa Ndoa.

**a. Muundo wa Mabaraza ya Jumuiya**

Baraza litaundwa na

i. Mwenyekiti;
ii. Makamu Mwenyekiti;
iii. Wajumbe wasiopungua watano (5) kwa kuzingatia jinsi bila kuathiri imani, mila na desturi ya Jumuiya husika; na
iv. Katibu atateuliwa na kamati au taasisi inayounda Jumuiya kwa mujibu wa taratibu za Jumuiya husika lakini hataruhusiwa kusaini Fomu Na. 3.

**b. Sifa za Wajumbe**

i. Wajumbe watapatikana kulingana na taratibu za Jumuiya husika;na
ii. Viongozi wa Jumuiya akiwemo Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu watapatikana kulingana na taratibu za Jumuiya husika.

**c. Majukumu**

i. Kuimarisha amani na utengamano katika Jumuiya husika kwa kuhakikisha migogoro inasuluhishwa kwa njia ya mazungumzo na kukubaliana;
ii. Kupokea na kusuluhisha mashauri ya migogoro ya ndoa;
iii. Kuandaa na kutoa barua ya wito;
iv. Kuendesha usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
v. Kutoa unasihi kwa wanandoa katika eneo husika;
vi. Kuelimisha wanandoa kuhusu malezi chanya ili kuimarisha makuzi na maendeleo ya mtoto katika ya familia;
vii. Kuwaelimisha wanandoa juu ya haki na wajibu wao kwa mujibu wa imani yao;
viii. Kusimamia makubaliano yaliyofikiwa na wanandoa katika usuluhishi ili kuimarisha mahusiano baina yao, familia na watoto;
ix. Kuwasilisha shauri la ndoa Mahakamani pale usuluhishi unaposhindikana kwa kujaza Fomu Na.3 kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ilivyoambatishwa

katika Mwongozo huu; na

x. Kujaza kwenye Rejista taarifa zote muhimu na kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa za mashauri yote ya Baraza kwa mamlaka husika.

**Kumbuka:** Ni takwa la kisheria kujaza fomu no 3 pale shauri linapopelekwa mahakamani, lakini kuambatisha muhtasari na barua kwenda mahakamani sio takwa la kisheria.

**d. Majukumu ya Katibu**

i. Kupokea mashauri na kuyasajili kwenye Rejista ya Mabaraza ya Ndoa;
ii. Kuandaa taarifa;
iii. Kuandaa muhtasari wa kikao;
iv. Kutunza kumbukumbu za vikao kwa mujibu wa taratibu za utunzaji wa nyaraka za umma; na
v. Kujaza Fomu Na. 3 na kuiwasilisha kwa Mwenyekiti kwa ajili ya kusainiwa.

e. **Uwajibikaji wa Baraza la Jumuiya**

Katika kuhakikisha Baraza linafanya kazi yake kiufanisi, litapaswa kuwajibika kwa viongozi wa Jumuiya husika ngazi ya juu, ambao watapaswa kutoa taarifa Wizara ya Katiba na Sheria.

# SEHEMU YA TATU
# UTARATIBU WA USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDOA

## 3.1. Maelezo

Sehemu hii inaainisha kanuni na maadili ya kuzingatiwa na Mabaraza na namna ya kushughulikia masuala ya ndoa katika Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa. Aidha, imeainisha utaratibu wa usuluhishi, hatua za usuluhishi, ratiba ya vikao vya usuluhishi na rufaa kwa kuzingatia Kifungu cha 104 cha Sheria ya Ndoa sura 29 pamoja na kanuni kuhusu mwenendo wa Mabaraza ya Usuluhishi za Mwaka 1971.

## 3.2. Maadili na Kanuni za Kuzingatiwa na Mabaraza

### 3.2.1. Wajumbe wa Baraza Wanapaswa Kuzingatia Kanuni Muhimu Zifuatazo:

i. Kuepuka matumizi ya sauti ya ukali, matusi, kejeli au dharau;
ii. Uwepo wa utulivu na amani wakati wote wa kuendesha usuluhishi na kudhibiti mihemko;
iii. Kuepuka kupendelea upande wowote;
iv. Kusikiliza mashauri kwenye chumba kwa kuzingatia usiri na faragha;
v. Kutoa uhuru na nafasi sawa ya kujieleza kwa wanandoa na familia;
vi. Kuendesha usuluhishi kwa busara, uaminifu na uadilifu;
vii. Kujiepusha na vitendo vya rushwa na kupokea zawadi;
viii. Gharama itozwe kwa shauri na sio kwa vikao, kama utaratibu huo upo lakini gharama isiwe kikwazo cha kumhudumia mteja;
ix. Kuheshimu mawazo ya kila mjumbe wa Baraza na wahusika wa shauri;
x. Kuwawezesha wanandoa kufikia maamuzi sahihi;
xi. Kusuluhisha na sio kutoa hukumu kama vile kutoza faini, kugawa watoto na mali;
xii. Kumchukulia kila mwanandoa kwa upekee wake; na
xiii. Endapo mwanandoa mmoja akifika mapema kabla ya mwingine basi asiruhusiwe kuingia ndani ya Baraza kabla ya mwenzake.

### 3.2.2. Namna ya Kuwasilisha Shauri Mbele ya Baraza la Usuluhishi

Kama ilivyoainishwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 239 ya Mwaka 1971 na katika Kanuni ya saba (7) kuhusu mwenendo wa Mabaraza ya Usuluhishi, mlalamikaji/mwanandoa anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa njia zifuatazo :-

i. Kuwasilisha yeye mwenyewe kwa njia ya mdomo au maandishi; na
ii. Kuwasilisha kupitia uongozi wa serikali za Mtaa/Kijiji, ofisi ya Ustawi wa Jamii, Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi, nk.

## 3.3. Taratibu za Uendeshaji wa Usuluhishi wa Ndoa

i. Katibu au Mjumbe atapokea ombi la muombaji na kumtaarifu mwenyekiti;
ii. Taarifa ya maandishi itatolewa kwa wote wanaohusika kwa kuwafahamisha tarehe, muda na mahali pa kufanyia kikao cha Baraza kwa kujaza Fomu Na.1;
iii. Baraza litoe fursa sawa ya kuwasikiliza wanandoa au familia;
iv. Baraza lifanye uchunguzi pale inapobidi ili kupata taarifa za kina;
v. Baraza likiona inafaa kulingana na mazingira na uzito wa shauri litaahirisha shauri na

kupanga tarehe nyingine ya kulisikiliza;

vi. Baraza litamwita mtu mwingine nje ya wanandoa anayeweza kusaidia kwenye usuluhishi endapo wataona inafaa;

vii. Baraza linaweza kuomba Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya itoe wito (summons) kwa mtu aliyekataa wito wa Baraza angalau mara tatu;

viii. Mawakili hawaruhusiwi kuwakilisha mtu yeyote katika Baraza la Usuluhishi wa Ndoa;

ix. Mwanandoa hatakuwa na haki ya kuwakilishwa na ndugu isipokuwa kwa ruhusa ya Baraza;

x. Iwapo wanandoa watamaliza mgogoro wao kwa kusuluhishwa na kukubaliana, Baraza litatunza kumbukumbu kwenye jalada la siri na kufunga shauri;

xi. Kujaza kwenye Rejista taarifa zote muhimu na kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa za mashauri yote ya Baraza kwa mamlaka husika;

xii. Baraza linaweza kupeleka taarifa ya pingamizi la ndoa inayokusudiwa kufungwa kwa Msajili wa Ndoa kujulisha ndoa hiyo ifungwe au isifungwe kwa kujaza Fomu Na. 2; na

xiii. Pale usuluhishi utakaposhindikana Baraza litashauri wahusika waende mahakamani kwa kuwajazia Fomu Na. 3 itakayosainiwa na Mwenyekiti wa Baraza.

### 3.4. Hatua za Uendeshaji na Usuluhishi wa Ndoa

i. Mwenyekiti atampa nafasi mlalamikaji kueleza malalamiko yake na kufuatiwa na mlalamikiwa;

ii. Wakati wa uendeshaji wa shauri, Baraza likiona inafaa na kwa ridhaa ya wanandoa/familia linaweza kuwasikiliza mmoja baada ya mwingine;

iii. Baada ya kusikiliza pande zote, Mwenyekiti wa Baraza atatoa nafasi kwa wajumbe wa Baraza kuwauliza wanandoa maswali ya ufafanuzi kama yapo;

iv. Baada ya wajumbe wa Baraza kusikiliza pande zote mbili watatoa ushauri kwa wanandoa;

v. Endapo muafaka haujapatikana Mwenyekiti ataahirisha kikao ili kuwapa wanandoa muda wa kutafakari;

vi. Wanandoa wapewe muda wa kutafakari ili kuwapa nafasi ya kutosha kuona umuhimu wa kupatana na kuepusha madhara za kuvunjika kwa ndoa; na

vii. Baraza litaahirisha shauri hilo na kupanga siku nyingine kwa kuzingatia maoni ya wajumbe.

### 3.5. Ratiba ya Vikao vya Usuluhishi

i. Hakuna idadi kamili ya vikao vya usuluhishi wa shauri la mgogoro wa ndoa; na

ii. Baraza litaangalia uzito na mazingira ya shauri lililoletwa mbele yake na kulipatia ufumbuzi kwa muda usiozidi miezi sita (6) baada ya kupokelewa.

### 3.6. MAOMBI YA TALAKA MAHAKAMANI

i. Iwapo usuluhishi utashindikana, Baraza litatoa fomu maalum (Fomu Na. 3) yenye maoni kuthibitisha kwamba limeshindwa kuwapatanisha wanandoa pamoja na sababu za kushindwa kuwapatanisha kama ilivyotajwa kwenye Nyongeza ya Kanuni kuhusu Mwenendo wa Mabaraza ya Usuluhishi za Mwaka 1971; na

ii. Fomu Na. 3 iwasilishwe mahakamani katika kipindi kisichozidi miezi sita (6) kama uthibitisho kuwa Usuluhishi umeshindikana.

# SEHEMU YA NNE
# MAJUKUMU YA WADAU

## 4.1. Maelezo

Sura hii inaainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika utekelezaji wa mwongozo na mchango wao katika masuala mazima ya ustawi wa familia na usuluhishi wa Ndoa. Ufanisi wa utekelezaji wa Mwongozo huu utategemea usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa wadau katika ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, sura hii inaainisha Taasisi za Umma na Dini, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla yatakavyoshiriki katika utekelezaji wa Mwongozo.

## 4.2. Majukumu

Majukumu ya kila mdau yameainishwa kama ifuatavyo : -

### 4.2.1. Ngazi ya Taifa

a. **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

i. Kuandaa mpango, bajeti na ratiba ya ziara ya usimamizi shirikishi katika Halmashauri za Mkoa husika;
ii. Kupokea na kutoa huduma za usuluhishi wa Ndoa kupitia Baraza la Usuluhishi la Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
iii. Kutoa elimu ya malezi ya watoto ndani ya familia kwa wanandoa kabla na baada ya ndoa kwa lengo la kuwapatia stadi za mahusiano kupitia stadi za mawasiliano baina yao;
iv. Kuandaa Rejista na kusambaza takwimu zinazohusiana na migogoro ya ndoa;
v. Kuandaa programu za kutoa elimu kwa jamii na kwa lengo la kupunguza na kuondoa migogoro ya ndoa katika familia;
vi. Kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wanandoa na famila;
vii. Kutoa elimu ya haki na wajibu kwa wazazi kuhusu malezi chanya, matunzo na ulinzi wa mtoto;
viii. Kuratibu na kutoa msaada wa kitaalam wa utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa;
ix. Kusimamia Utekelezaji wa Mwongozo, Kanuni na Taratibu za Usuluhishi wa Ndoa;
x. Kudhibiti maudhui yanayokuwa kwenye mitandao, vyombo vya usafiri vya umma na maeneo ya wazi ili kunusuru uvunjifu wa maadili yanayoweza kusababisha migogoro ya ndoa;
xi. Kutoa msaada wa kitaalam na kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Jamii, wadau na wajumbe wa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Jumuiya kuhusu Mwongozo, Kanuni na Taratibu za Usuluhishi wa Ndoa;
xii. Kufanya usimamizi shirikishi kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI, Wizara za kisekta, washirika wa utekelezaji na wadau wa maendeleo;
xiii. Kufanya tafiti zinazohusu migogoro ya ndoa;
xiv. Kutafuta rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Mwongozo huu;
xv. Kuhuisha mfumo wa taarifa za Usuluhishi wa Ndoa kutoka OR - TAMISEMI;
xvi. Kutumia taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika kupanga mipango na bajeti ya afua za kuimarisha huduma za usuluhishi nchini;

xvii. Kujenga mahusiano na wadau wa ndani na nje ili kutoa huduma bora za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
xviii. Kufuatilia, kutathmini na kuboresha utekelezaji wa Mwongozo;
xix. Kuandaa kitini cha mafunzo kwa Mabaraza ya usuluhishi wa Ndoa;
xx. Kuanzisha na kutekeleza programu za elimu kwa jamii kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa;
xxi. Kutoa taarifa kwa mashauri ya ndoa katika Mahakama pale ambapo usuluhishi umeshindikana;
xxii. Kuchapisha na kusambaza Mwongozo huu kwa Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa ya Kata na Jumuiya, wadau, na watendaji wa Serikali;
xxiii. Kuandaa Rejista za usuluhishi wa Ndoa  na kusambaza taarifa kwa wadau mbalimbali;
xxiv. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH) kupitia maudhui ya mitandao ya kijamii kwa lengo la kuboresha taasisi ya ndoa;
xxv. Kuandaa vikao vya wadau kwa lengo la kuboresha taasisi ya ndoa; na
xxvi. Kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo yanayohusiana na taasisi ya ndoa na familia pale inapohitajika.

**b. Wizara ya Afya (WA)**

i. Kutoa huduma za matibabu kwa haraka kwa wahanga wa migogoro ya ndoa;
ii. Kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa manusura wa vitendo vya ukatili unaotokana na migogoro ya ndoa ; na
iii. Kutoa rufaa kwenda ngazi husika kwa manusura wa vitendo vya ukatili.

**c. Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR -TAMISEMI)**

i. Kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Katiba na Sheria,Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa  katika Halmashauri na Kata;
ii. Kufanya usimamizi shirikishi kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Wizara za kisekta na wadau wa maendeleo katika Halmashauri na mabaraza ya usuluhishi ya kata na jumuiya;
iii. Kushirikisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Usuluhishi wa Ndoa katika Mabaraza ya usuluhishi ya Kata na Jumuiya;
iv. Kupokea taarifa za usuluhishi wa migogoro kutoka Sekretarieti za Mikoa;
v. (v) Kutumia taarifa za usuluhishi katika kupanga mipango na bajeti ya ufuatiliaji wa afua za kuimarisha huduma za usuluhishi katika ngazi za Sekretarieti ya Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (MSM);
vi. Kutafsiri Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa kwa ajili ya utekelezaji katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM);
vii. Kusimamia usambazaji wa Mwongozo huu;
viii. Kuwajengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu Mwongozo huu na;
ix. Kusimamia utekelezaji wa programu za elimu kwa jamii kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa na familia katika Halmashauri.

**d. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (WMN)**

i. Kutoa elimu na ushauri kwenye jamii juu ya masuala ya ndoa pamoja na ukatili wa kijinsia wenye asili ya jinai; na
ii. Kutoa rufaa kwenda ngazi husika kwa manusura wa vitendo vya ukatili.

iii. Kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria dhidi ya watu wanaofanya ukatili

**e. Wizara ya Katiba na Sheria (WKS)**

i. Kufanya mapitio ya sheria na kanuni zinazosimamia Usuluhishi wa Ndoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha taasisi ya ndoa;
ii. Kushiriki kwenye kuhuisha Mwongozo huu;
iii. Kufanya usimamizi shirikishi wa utendaji wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara za kisekta na wadau wa maendeleo;
iv. Kuratibu watoa huduma za kisheria na huduma za msaada wa kisheria katika migogoro ya ndoa;
v. (v) Kuunda, kuyatambua na kuidhinisha Mabaraza ya Ndoa kwa kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.
vi. Kushirikiana na Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Kutoa elimu ya Sheria ya ndoa na usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa mawakili, wanasheria, wasaidizi wa kisheria na wananchi;
vii. Kuanzisha na kuendesha Mahakama za familia; na
viii. Kuratibu uhuishaji wa taarifa za usajili wa ndoa na talaka ili kutengeneza afua za kupunguza migogoro ya ndoa.
ix. Kupokea taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kutoka Mabaraza ya Usuluhishi ya kijumuiya
x. Kupokea nakala za taarifa usuluhishi wa migogoro ya ndoa kutoka OR-Tamisemi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii.
xi. Kutunza daftari/ Rejista ya Mabaraza ya Jumuiya katika masuala ya usuluhishi

### 4.2.2. Sekretarieti za Mikoa

i. Kuwezesha na kutoa ushauri wa kitaalamu katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusiana na Sheria na mwongozo wa Mabaraza ya usuluhishi wa Ndoa kama ilivyoandaliwa na Wizara;
ii. Kupokea na kuchambua taarifa kutoka katika Halmashauri za mkoa husika;
iii. Kuwasilisha taarifa za Usuluhishi wa Ndoa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
iv. Kuratibu wadau wanaoshirikiana na Serikali katika kutoa huduma za usuluhishi wa masuala ya ndoa;
v. Kupokea na kuchambua taarifa za migogoro ya ndoa kutoka kwenye ngazi za Halmashauri; na
vi. Kuwasilisha taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

### 4.2.3. Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji

i. Kuandaa mpango, bajeti na ratiba ya ziara ya usimamizi shirikishi katika Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Jumuiya;
ii. Kushirikiana na wadau kutafuta rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa afua za kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
iii. Kuandaa taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na kuziwasilisha Sektrarieti ya Mkoa;
iv. Kushirikisha taarifa za huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwa wadau ili kuboresha huduma;

v. Kuteua katibu wa Baraza la Kata la Usuluhushi;
vi. Kutoa ushauri wa kitaalamu na kujenga uwezo kwa Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Jumuiya;
vii. Kuhakikisha Mabaraza ya Ndoa ya Kata na ya Jumuiya yanafanya kazi za usuluhishi kwa weledi kwa kufanya usimamizi saidizi kupitia maafisa ustawi wa jamii katika Halmashauri husika.
viii. Kuwahamasisha wanandoa na familia kwenda Baraza la Usuluhishi la Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata na Jumuiya;
ix. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa katika Halmashauri;
x. Kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wanandoa na familia na kuratibu wadau mbalimbali wanaoshirikiana na serikali katika kutoa huduma za ndoa; na
xi. Kuyawezesha mabaraza ya kata kuhifadhi na kutunza kumbukumbu (ununuzi wa makabati, majalada nk).

### 4.2.4. Ofisi ya Mtendaji wa Kata

i. Kupokea migogoro ya ndoa kwa mujibu wa Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa;
ii. Kuimarisha amani na utengamano na kuhakikisha migogoro inatatuliwa kwa njia ya mazungumzo;
iii. Kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia/watoto kwa Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto;
iv. Kutoa rufaa ya migogoro ya ndoa inayohitaji msaada wa Kisheria kwenda taasisi na mashirika yanayotoa msaada wa kisheria;
v. (v) Kusimamia uandaaji na kuwasilisha taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwenda Halmashauri;
vi. Kushiriki Mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Mwongozo wa huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
vii. Kutoa elimu kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa na familia katika jamii; na
viii. Kutoa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wanandoa na famila.

### 4.2.5. Ofisi ya Mtendaji wa Mtaa/Kijiji

i. Kupokea mashauri ya migogoro ya ndoa kwa mujibu wa Mwongozo wa Taifa wa Usuluhishi wa Ndoa;
ii. Kuimarisha amani na utengamano na kuhakikisha migogoro inatatuliwa kwa njia ya mazungumzo;
iii. Kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia/watoto kwa Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto;
iv. Kusimamia uandaaji na kuwasilisha taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa kwenda kata;
v. Kushiriki Mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Mwongozo wa huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa; na
vi. (Kutoa msaada wa awali wa kisaikolojia na kijamii kwa wanandoa na familia.

### 4.2.6. Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

i. Kushirikiana na Serikali katika ngazi zote katika utekelezaji wa afua za huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
ii. Kushiriki katika ufuatiliaji, tathmini na mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
iii. Kushiriki kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa;

iv. Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Mwongozo wa Taifa wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
v. Kuwezesha na kushiriki mikutano ya mapitio ya Mwongozo wa Taifa wa usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
vi. Kutoa msaada wa kitaalamu ili kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Jamii, wajumbe wa mabaraza na wadau wengine wanaohusika na usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
vii. Kushiriki katika ziara za usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa afua za huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
viii. Kushiriki katika kuandaa taarifa za usimamizi shirikishi na kushirikisha mamlaka husika;
ix. Kutumia taarifa za migogoro ya ndoa kuandaa mipango na bajeti za afua za kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
x. Kushiriki na kuwezesha programu za kutoa elimu kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa na familia katika jamii;
xi. Kuunganisha wanandoa na mabaraza ya usuluhishi wa Ndoa ;
xii. Kutoa msaada wa kitaalam na wa kifedha katika utekelezaji wa Mwongozo wa mabaraza ya usuluhishi wa Ndoa;
xiii. Kutoa ushauri na msaada wa kisheria wa masuala ya ndoa na familia;
xiv. Kuingiza kwenye mipango yao na kushiriki katika tafiti za kupunguza migogoro ya ndoa; na
xv. Kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma za utatuzi wa migogoro ya ndoa.

### 4.2.7. Taasisi za Dini

i. Kutoa elimu kuhusu kuimarisha mahusiano ya ndoa na familia katika jamii;
ii. Kutoa elimu ya kiimani na kijamii ya masuala ya huduma za Usuluhishi wa Ndoa kwa waumini/washiriki kabla na baada ya migogoro;
iii. Kutoa huduma za usuluhishi na upatanishi wa migogoro ya ndoa;
iv. Kuwauganisha wanandoa wenye migogoro ya ndoa na Mabaraza ya Kata na Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
v. (v)Kutoa taarifa Polisi kuhusu migogoro ya ndoa yenye asili ya jinai;
vi. Kushiriki mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu Sheria, Kanuni na Mwongozo wa huduma ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa;
vii. Kutoa taarifa za migogoro ya ndoa kwa mamlaka husika kwa mujibu wa taratibu;
viii. Kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana orodha ya Mabaraza ya Jumuiya ya Usuluhishi mapya kwa ajili ya kutambuliwa rasmi au kupewa mamlaka ya usuluhishi kisheria; na
ix. Kuaandaa programu za mafunzo na ushauri nasaa kwa wanaoingia katika ndoa

### 4.2.8. Jamii

i. Kuanzisha afua za kijamii za kuondoa migogoro ya ndoa katika jamii;
ii. Kuendeleza mila na tamaduni chanya zinazopunguza migogoro ya ndoa kabla na baada ya ndoa;
iii. Kutoa taarifa za migogoro ya ndoa kwa mamlaka husika;
iv. Kutoa ushauri kwa wanandoa na familia zilizo katika migogoro ya ndoa; na
v. Kushiriki na kutoa maoni katika mikutano mbalimbali.

### 4.2.9. Familia/Wanandoa

i. Kuimarisha mahusiano baina ya wanandoa na familia;

ii. Kutoa malezi chanya kwa watoto kwa kuwapa stadi za Maisha;
iii. Kutoa taarifa za migogoro ya ndoa kwa mamlaka husika; na
iv. Kujielimisha na kutafuta suluhu ya migogoro.

### 4.3. Wasaidizi wa Kisheria/Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii

i. Kutoa msaada wa awali wa kisheria kuhusiana na masuala ya ndoa na migogoro ya ndoa;
ii. Kufanya usuluhishi wa awali kwa wanandoa wenye changamoto za ndoa;
iii. Kuwaunganisha na kuwaelekeza wanandoa mahali sahihi kwa msaada wa huduma nyingine za ushughulikiwaji wa migogoro ya ndoa; na
iv. Kutoa msaada wa awali wa kisaikolojia.

### 4.4. Msajili wa Vizazi na Vifo (RITA)

i. Kusajili na kutoa vyeti vya ndoa na talaka

## SEHEMU YA TANO
## USIMAMIZI SHIRIKISHI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 5.1. Maelezo

Sehemu hii inaelezea mchakato na utaratibu wa usimamizi shirikishi, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utendaji wa Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa katika ngazi ya Baraza la Usuluhishi la Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya.

### 5.2. Usimamizi Shirikishi

Usimamizi shirikishi utafanyika katika Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya ikihusisha timu za utendaji za Halmashauri husika ili kuyajengea uwezo Mabaraza haya. Aidha, usimamizi shirikishi utafanyika angalau mara mbili kwa mwaka. Usimamizi shirikishi wa timu ya wataalamu kutoka ngazi ya Taifa au Mkoa utafanyika endapo kutatokea uhitaji maalum wa zoezi hilo.

### 5.3. Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanyika katika Baraza la Kamishna, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya. Ufuatiliaji huu utafanyika mara mbili kwa mwaka ambapo katika Baraza la Kamishna, ufuatiliaji utafanywa na kamati MAALUM ambayo itaundwa na Katibu Mkuu - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Kamati hiyo itashirikisha wadau wa kisekta wakiwemo, Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Viongozi wa Dini. Vilevile, timu za utendaji za Halmashauri husika zitafanya ufuatiliaji katika Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya. Aidha, ufuatiliaji katika ngazi za Mabaraza ya Kata na Jumuiya utafanywa na timu ya wataalam kutoka ngazi ya Taifa au ngazi ya Mkoa kadri itakavyoonekana inafaa.

### 5.4. Utoaji wa Taarifa

Utoaji wa taarifa za usuluhishi wa migogoro ya ndoa utafuata utaratibu ufuatao : -

i. Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Mabaraza ya Jumuiya yatawasilisha taarifa katika mamlaka zao za juu za kiutendaji. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria itakusanya taarifa husika kila robo mwaka ;
ii. Mabaraza ya Kata yatawasilisha taarifa zao kila robo mwaka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika. Aidha, taarifa hizo zitawasilishwa Sekretarieti ya Mkoa na kutumwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI ; na
iii. Ofisi ya Rais-TAMISEMI watawasilisha taarifa katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na watawasilisha nakala Wizara ya Katiba na Sheria

**Kumbuka:** Zoezi la utoaji taarifa litafanyika na kuwasilishwa kwenye ngazi husika kwa kila robo mwaka kwa kutumia fomu maalum zilizoambatanishwa kwenye mwongozo huu.

### 5.5. Tathmini

Tathmini itafanyika katika ngazi ya Baraza la Kamishna, ngazi ya Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Jumuiya. Tathmini itafanyika kila baada ya miaka mitatu (3) ili kuweza kubaini mafanikio, changamoto na mambo mazuri ya kuendelezwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wataandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ambao utaweka viashiria vya kupima matokeo ya utekelezaji wa mwongozo huu.

# VIAMBATISHO

## 6.1. Fomu Na.1. Fomu ya Wito

**Fomu na.1**

**BARAZA LA KUSULUHISHA MASHAURI YA NDOA LA**

……………………………………………………………………………………………………….

*(Taja aina ya Baraza na mahali lilipo)*

**BARAZA hili limepokea shauri la ndoa lililoletwa**
na
……………………………………………………………………………………………..

*(Taja jina la aliyepeleka shauri Barazani)*

kuhusu ndoa au inayokusudiwa kufungwa baina ya

…..………………………………………………………………………………………………
*(Taja jina la mume)*
na
…..…………………………………………………………………………………………..
*(Taja jina la Mke)*

SHAURI hilo linahusu……..…………………………………………………………….....

...…………………………………………………………………………………...……
*(Toa maelezo ya shauri)*

**HII NI TAARIFA YA MKUTANO** wa Baraza ambao utaanza saa………………siku ya tarehe …………………....na Mahali pa mkutano ni………………………………nawe uliyeletewa taarifa hii unatakiwa uhudhurie mkutano huo uliotajwa hapo juu.

**KUMBUKA KWAMBA** usipohudhuria mkutano huo uliotajwa au mwingine utakaofuata, Baraza hili itaiomba Mahakama itoe kuitwa shaurini kwa ajili ya kukutaka uhudhurie kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha tatu (3) cha Fungu la 104 la Sheria ya Ndoa.

..…………………………………………
*(Saini) Mwenyekiti /Makamu wa Mwenyekiti/ Mjumbe wa Baraza*

Tarehe ………………..…………

### 6.2. Fomu Na.2: Pingamizi la Ndoa

**Fomu na.2**

**BARAZA LA KUSULUHISHA MASHAURI YA NDOA LA**

………………………………………………………………………………………………..

*(Taja aina ya Baraza na mahali lilipo)*

BARAZA hili limepokeleka shauri la ndoa lililowasilishwa Barazani kwa kufuata masharti ya Fungu la 21(1) (b) la Sheria ya Ndoa, nalo linahusika na ndoa inayokusudiwa kufungwa baina ya………………………………………………………..

…..……………………………………………………………………………………………
*(Taja jina la mwanaume anayekusudia kufunga ndoa)*

*Na*

……………………………………………………...
*(Taja jina la mwanamke anayekusudia kufunga ndoa)*

na linatokana na taarifa ya pingamizi ya ndoa iliyotolewa na…………………………

…………………………………………………………………………………………………..
*(Taja Jina la Mpinzani)*

INATHIBITISHWA kwamba uamuzi wa baraza juu ya shauri hilo ni kuwa ndoa hiyo inayokusudiwa kufungwa inaweza kufungishwa/isifungishwe.

…..……………………………..
*(Saini) Mwenyekiti/Makamu wa Mwenyekiti*
*Mjumbe wa Baraza*

Tarehe …………………………………

### 6.3. Fomu Namba 3: Rufaa Mahakamani

**Fomu Na.3**

**BARAZA LA USULUHISHI WA MASHAURI YA NDOA**

**AINA YA BARAZA** ……………………………………………………………………..

Kutokana na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, vifungu nambari 102, 103, na 104 Baraza hili limepokea na kusikiliza shauri la ndoa kati ya

…..…………………………………..  ………………………………………..

*(Taja Jina la Mume)* *(Taja Jina la Mke)*

*(Taja Jina la Aliyepeleka Shauri Barazani)*…………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

Inathibitishwa kwamba, Baraza hili limeshindwa kabisa kuwasuluhisha watu hao wawili, yaani mume na mkewe, kwahiyo maoni ya Baraza hili ni kuwa:

…..……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
…

*(Taja mapendekezo yoyote ya Baraza kuhusu shauri hili)*

…..………………………………………………………………………………...............
......................................................................................................................................
.........................................................

…..……………………………..

(*Saini) Mwenyekiti/Makamu wa Mwenyekiti*
*Mjumbe wa Baraza*

Tarehe ……………………..

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**REJISTA YA USULUHISHI WA MASHAURI YA NDOA NA FAMILIA**

**Mkoa** .............................. **Wilaya**...............................**Kata** ........................................

| NA | KUMB NA: | TAREHE | MAJINA YA WANANDOA | UMRI | JINSIA | IDADI YA WATOTO | DINI | KABILA | ELIMU | KAZI | MWAKA WA KUFUNGA NDOA | MAHALI ANAPOISHI | AINA YA NDOA | TATIZO | HATUA ZILIZO CHUKULIWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | |

## MSIMBO/KIELELEZO

| JINSIA | ELIMU | DINI | KAZI | UMRI | TATIZO | HATUA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. KE<br>2. ME | 1. SIJASOMA<br>2.MSINGI<br>3.SEKONDARI FORM 1-4<br>4.SEKONDARI FORM 5-6<br>5.CHETI<br>6.DIPLOMA<br>7.SHAHADA<br>8.SHAHADA YA UZAMILI<br>9.SHAHADA YA UZAMIVU | 1.MUISLAM<br>2.MKRISTO<br>3.NYINGINEZO | 1.MKULIMA<br>2.MFANYABIASHARA<br>3.AMEAJIRIWA SERIKALINI<br>4.AMEJIAJIRI<br>5.AMEAJIRIWA SEKTA BINAFSI<br>6.HAJAAJIRIWA | 1.CHINI YA 18<br>2.18-24<br>2.25-35<br>3.35-44<br>4.45-54<br>5.55-64<br>6.65+ | 1.KUTELEKEZWA<br>2.UKATILI<br>3. KUKOSA TENDO LA NDOA<br>4. KUKOSA UAMINIFU KWENYE NDOA<br>5.USHIRIKINA<br>6.ULEVI<br>7. UGO NJWA<br>8. NYINGINEZO | 1.WAMESULUHISHWA<br>2. RUFAA NGAZI YA JUU<br>3. RUFAA MAHAKAMANI<br>4.KUTENGANI HWA KWA MUDA |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

## FOMU YA UTOAJI WA TAARIFA ZA USULUHISHI WA NDOA KATIKA MABARAZA KWA ROBO MWAKA.

Julai-Septemba ☐ Oktoba-Desemba ☐ Januari-Machi ☐ April -Juni ☐

**MWAKA……………….**
**JINA LA BARAZA…………………………………………**
**MKOA……………….HALMASHAURI ……………..KATA**
**AINA YA BARAZA:** Weka tiki Panapostahili
Baraza la Kamishna wa Ustawi wa Jamii ☐
Baraza la Jumuiya ☐ Taja ……………….
Baraza la Kata ☐

| N | Idadi ya mashauri yaliyopokelewa | Idadi ya mashauri yaliyosuluhishwa | Idadi ya mashauri Yaliyopelekwa ngazi ya juu katika taasisi husika | Idadi ya mashauri yaliyopelekwa mahakamani | Idadi ya mashauri yanayoendelea | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Chini ya miezi 3 | Zaidi ya miezi 3 |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

## FOMU YA UTOAJI WA TAARIFA ZA USULUHISHI WA NDOA KATIKA MABARAZA YA JUMUIYA KWA ROBO MWAKA.

Julai-Septemba ☐ Oktoba-Desemba ☐ Januari-Machi ☐ April -Juni ☐

**MWAKA**…………..
**JINA LA BARAZA**………………………..
**MKOA**…………………..**HALMASHAURI**…………………………..**KATA**……………….
**AINA YA BARAZA:** Weka tiki Panapostahili
Baraza la Jumuiya ☐ Taja…………………

| N | Idadi ya mashauri yaliyopokelewa | Idadi ya mashauri yaliyosuluhishwa | Idadi ya mashauri Yaliyopelekwa ngazi ya juu katika taasisi husika | Idadi ya mashauri yaliyopelekwa mahakamani | Idadi ya mashauri yanayoendelea | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Chini ya miezi 3 | Zaidi ya miezi 3 |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |



Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wanawake na Makundi Maalum,
S.L.P 573, DODOMA

